# TIMER NATIONAL SERIES {7}
# MAJARIBIO YA MTIHANI
## DARASA LA SABA KISWAHILI

CODE0072021

Muda: Saa 1 Dak 40

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya uliyopewa.***

Kila __1__ alipigwa na __2__ alipozipokea habari hizo. Zilikuwa ni habari za kutisha. __3__ watu sitini walikuwa wameaga dunia __4__ na ulevi wa pombe __5__ . Lawama na __6__ zilielekezwa viongozi wa __7__ hasa ilipodhihirika kuwa mgema alikuwa amekwepa __8__ . Serikali nayo ilichukua hatua za __9__ ili kuzuia jangwa kama __10__ kutokea tena.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. mdhamini | B. mzalendo | C. mlowezi | D. mwanzilishi |
| 2. | A. butaa | B. chakari | C. huzuni | D. bashasha |
| 3. | A. Karibu | B. Kila | C. Hao | D. Wapo |
| 4. | A. kwa | B. kutokana | C. kulingana | D. katika |
| 5. | A. haramu | B. ghali | C. chafu | D. baya |
| 6. | A. heko | B. laani | C. shutuma | D. hongera |
| 7. | A. siasa | B. kidini | C. ujamii | D. utawala |
| 8. | A. kutozwa | B. kutiwa mbaroni | C. kupigwa kalamu | D. kula mulungula |
| 9. | A. polepole | B. nguvu | C. siasa | D. dharura |
| 10. | A. ile | B. hio | C. hilo | D. hiyo |

Watu wengi __11__ kwamba watoto aghalabu hufuata __12__ ya wazazi __13__ . Mzazi __14__ na hulka njema, pana __15__ watoto wawe vivyo hivyo kwani wahenga waliamba mwana hutazama kisogo cha ninake.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 11. | A. husadiki | B. huteta | C. huapa | D. hugamba |
| 12. | A. nyayo | B. mienendo | C. mwenendo | D. mielekeo |
| 13. | A. zao | B. yao | C. wao | D. wake |
| 14. | A. akiwa | B. aliye | C. anaye | D. mwenye |
| 15. | A. uwezo | B. uwezekano | C. tetesi | D. ukweli |

***Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu swali kulingana na maagizo.***

16. Iwapo juzi ilikuwa siku ya Ijumaa, mtondo itakuwa siku ipi?
    A. Jumatatu B. Jumanne
    C. Jumatano D. Jumapili

17. Ni sentensi ipi inayoonyesha kivumishi kimilikishi?
    A. Kiatu hiki ni kipya.
    B. Kijana mtiifu hupendeza.
    C. Alifurahi bali hakucheka.
    D. Dukani kwenu ni kuzuri.

18. Ni sentensi ipi inayoonyesha ki ya masharti?
    A. Tukienda tutawapata.
    B. Kila mtu ana furaha.
    C. Tutakapokuwa tukila watatoka.
    D. Walinunua kiatu kizuri.

19. Ni nini ufupisho wa babu zake?
    A. Babake B. Babuko
    C. Babuye D. Babuze

20. Andika wingi: **Ua unapendeza.**
    A. Nyua zinapendeza
    B. Maua yanapendeza
    C. Ua zinapendeza
    D. Maua zinapendeza

21. Ni sentensi ipi iliyo na **"kwa"** ya nia?
    A. Tulimkaribisha kwa furaha.
    B. Ninatoka kwa mjomba wangu.
    C. Tulimtembelea kwa kumjulia hali.
    D. Alitumia msumeno kwa kukereza mba

**22.** Andika katika wingi.
**Ua hilo lilimea karibu na ua ule mrefu.**
A. Nyua hizo ndefu zilimea karibu na maua hayo.
B. Maua hayo yalimea karibu na nyua zile ndefu.
C. Maua hayo yalimea karibu na nyua hizo ndefu.
D. Maua hayo yalimea karibu na maua yale marefu.

**23.** Kamilisha sentensi.
Sikujui _______ alikohamia.
A. kule B. wewe
C. mle D. hapo

**24.** Kamilisha tashbihi:
**Watu hao wanashabihiana kama**
A. chanda na pete
B. kalamu na karatasi
C. ardhi na mbingu
D. shilingi kwa ya pili

**25.** Mtu anayebeba mizigo kwa malipo huitwaje?
A. Kuli B. Hamali
C. Utingo D. Machenga

**26.** Neno lipi kati ya haya linaonyesha kitenzi?
A. Chupa B. Tunda
C. Mto D. Langu

**27.** Tegua kitendawili:
**Akilia tunafurahi.**
A. Maji B. Mto
C. Moto D. Mvua

**28.** Ni sentensi ipi sahihi?
A. Mgeni aliingia ndani mwa nyumba.
B. Mgeni aliingia katika nyumbani.
C. Mgeni aliingia katika nyumba.
D. Mgeni aliingia nyumba.

**29.** **Mtoto huyu ana kichwa kikubwa.** Maana yake ni
A. ana wivu
B. ana kiburi
C. ana uzembe
D. ana tamaa

**30.** Kamilisha methali.
_______ huwa mwema.
A. Mui B. Mwizi
C. Mchawi D. Mtoro

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 hadi 40.</u>***

Mzaha mzaha hutunga usaha. Nao usaha hunuka na una aibu. Aibu nayo huleta majuto na kushuka kwa heshima. Afanyaye jambo lenye aibu haheshimiki.

Kwa miaka mingi, wimbo wa uhifadhi wa mazingira umekuwa vinywani mwa wengi. Kila kukicha tukaelezewa tujiepushe na ukataji ovyo wa miti. Tukahimizwa na kuelemishwa kuwa iwapo tutaikata miti, basi tuipande mingine papo hapo.

Tulielezwa tele kuhusiana na utumiaji mbolea asilia ambayo haina madhara katika udongo wetu. Hatukukosa wosia na nasaha kuhusiana na mbinu mwafaka za kilimo ili kuepuka au kuzuia mmomonyoko wa udongo. Lakini yote hayo, wengi wetu tuliyatemea mate. Ikawa ni sawa na kumwashia kipofu taa. Ni sawa na kumpigia mbuzi gitaa.

Tulishauriwa kutoichafua mito yetu lakini tukaigeuza kuwa mabomba ya uchafu. Ni jambo la kusikitisha kuona baadhi ya wawekezaji wakielekeza mifereji ya maji taka kutoka viwandani mwao hadi mitoni au maziwani.

Si ajabu tena kuona mifereji kutoka vyooni ikielekezwa hadi mitoni. Isisahaulike maji ya mito yiyo hiyo yanatumiwa na binadamu, mifugo, ndege na wanyamapori.

Ukizuru mitaa yetu, washangaa kuona kuwa nusura katika kila sehemu wazi, imegeuzwa kuwa biwi la takataka. **<u>Mirundika ya takataka inayonuka fee imesimama kwa aibu kila mahali</u>**. Ni aibu na fedheha yetu hiyo. Kivuli hicho cha fedheha kinatuandama popote tuendapo licha ya kujiita wastaarabu na wajuaji.

Matokeo ya hayo yote ni masaibu tele yanayotufuata. Hatuachi kulalamika kutokana na maradhi ya kila aina. Tutaepukaje maradhi ilhali baadhi ya mboga tunazotumia hunyunyiziwa maji ya takataka!

Maradhi yatokanayo na uchafuzi wa hewa limekuwa jambo la kawaida aushini mwetu. Mikurupuko ya ndwele kama vile kipindupindu si jambo geni maishani mwetu. Kweli usaha hunuka. Nayo majuto ni mjukuu mwishowe huja kinyume.

Uhaba wa chakula ni tisho kubwa kwetu. Kutokana na mbinu mbovu za kilimo, mashamba yetu yanarudi kushindwa kutosheleza mahitaji yetu.

Mito yetu nayo inazidi kuakuka. Viumbe vya majini vinazidi kudidimia. Kisa na maana, misitu inazidi kudidimia nayo mito inazidi kuchafuliwa. Mingi yao inaweza kuitwa mito ya sumu.

Maafa hayo yote yanatokana na miaka mingi ya mzaha. Mzaha dhidi ya mazingira yetu. Mambo hayo yanastahili kuchukuliwa kwa uzito ufaao **tukaya dhararisha**. Nayo matokeo ndiyo haya. Maafa yanayotishia sio maisha yetu tu bali na ya vizazi vijavyo.

Yafaa tuchukue hatua mwafaka, imara na za dharura. Tuirejeshe hali ya zamani ili tuweze kufurahia mandhari yetu.

---

**31.** Kulingana na ufahamu, majuto hutokana na
A. mzaha
B. aibu
C. kushuka kwa hadhi
D. usaha

**32.** Kwa nini mwandishi anafananisha hali husika na kuwashia kipofu taa?
A. Kipofu hajui faida ya taa.
B. Mawaidha yaliyotolewa yaliwajaa watu.
C. Mawaidha yaliyotolewa hayakuwanufaisha waliotengwa.
D. Mawaidha hayo yalikuwa duni.

**33.** Kulingana na ufahamu, mmomonyoko wa udongo husababishwa na
A. mvua nyingi.
B. uchafuzi wa mito.
C. utumiaji wa mbolea asilia.
D. njia duni za kilimo.

**34.** **Mirundiko ya takataka ....imesimama kwa aibu** inamaanisha
A. mazingira yetu machafu yanatuaibisha.
B. takataka hizo zinaona aibu.
C. watu wanaona aibu kutupa takataka.
D. takataka nyingi zinaaibisha.

**35.** Kwa nini mwandishi anasema, majuto ni mjukuu?
A. Uharibifu wa mazingira tuliotekeleza hapo awali unatudhuru leo hii.
B. Uharibifu wa mazingira wa leo hii unatuangamiza.
C. Tunajutia uajibikaji wetu wa siku za hapo nyuma.
D. Tunazidi kuharibu mazingira licha ya maafa ya jambo hilo.

**36.** Ukataji ovyo wa miti husababisha yafuatayo ila
A. mmomonyoko wa udongo.
B. ueneaji wa jangwa.
C. uchechefu wa chakula.
D. ugonjwa wa kipindupindu.

**37.** Ni yapi matokeo ya uchafuzi wa mazingira?
A. Maradhi, uhaba wa chakula, uchafu wa uimarikaji wa uchumi.
B. Ndwele, aibu, uchechefu wa chakula na mmomonyoko wa udongo.
C. Magonjwa, usaha, ukuaji wa viwanda, vifo vya viumbe na aibu.
D. Mmomonyoko wa udongo, vifo vya viumbe, maradhi, kunawiri kwa biashara.

**38.** Tatizo la mazingira linatishia
A. kutuangamiza sote binadamu.
B. kuangamiza viumbe vyote vya sasa.
C. kuangamiza viumbe vyote vya sasa na vya siku zijazo.
D. kuangamiza tamaduni zetu.

**39.** Mandhari ina maana ya
A. sherehe
B. sura ya mahali
C. matembezi
D. hali ya hewa

**40.** Ufahamu huu unatoa ujumbe upi?
A. Maafa ya kutohifadhi mazingira.
B. Maafa ya mmomonyoko wa udongo.
C. Aibu ya usaha.
D. Hasara za mzaha.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 hadi 50.***

Ni jambo lisilopingika kuwa, elimu ni ufungo wa maisha. Aidha, elimu ni nguzo imara ya kuegemea maishani. Hata hivyo, yafaa ifahamike kuwa elimu itamfaidi mmiliki wayo yule ambaye ataitumia kwa ufasaha. La muhimu zaidi, yule ambaye ataitumia kwa nidhamu, hekima na heshima.

Haijalishi iwapo mahuluki ameyasoma matopa ya vitabu. Haijalishi amefikia kiwango kipi au anazo shahada zipi: Iwapo hana adabu, heshima, nidhamu na uajibikaji, elimu yake haijakamilika. Elimu hiyo yote si lolote si chochote. Elimu yake itakuwa kama pambo wala si **lebasi**. Pambo haliwezi kusitiri mtu. Hiyo ni kazi ya nguo.

Ni fedheha kuwaona baadhi ya insi wakichawiza kuwa wameelimika ilhali wanazo fuska. Heshima kwao ni **mwiko**. Adabu kwao ni neno geni. Ukweli ni kuwa elimu hiyo yao haina faida kwa walimwengu. Mwalimu wangu wa zamani alinieleza kuwa kumiliki elimu ya aina hiyo ni sawa na kufunga tai huku mtu akiwa uchi wa mnyama.

Ni jambo aula mtu kuonyesha elimu yake kwa vitendo. Vitendo vya yeyote aliye na elimu vinafaa viwe na mwelekeo na vya kutamanika. Vionyeshe ustaarabu wala si ushenzi. Aidha ifahamike kuwa elimu si ya vitabu tu. La hasha! Ipo pia elimu dunia. Sharti elimu yetu ituwezeshe kutafakari ya dunia.

---

**41.** Elimu bora ni ipi?
A. Ya chuo kikuu
B. Yenye uajibikaji
C. Inayoheshimiwa
D. Ya ngumbaro

**42.** Mtu hutajika ameelimika ikiwa
A. amesoma matopa ya vitabu.
B. ana msururu wa shahada.
C. ana fuska.
D. ana ustaarabu.

**43.** Ni kweli kusema
A. yeyote aliye na elimu ni mustaarabu.
B. asiye na elimu ni mshenzi.
C. elimu ndiyo ufunguo wa maisha.
D. matendo mema hupita elimu.

**44.** Kisawe cha **lebasi** ni
A. nguo
B. elimu
C. pambo
D. silabasi

**45.** Lengo kuu la elimu ni lipi?
A. Kumtajirisha mmiliki
B. Kuwajibika
C. Kusifika kwa mmiliki
D. Kuelewa kufanya kazi tofauti

**46.** **"Ni jambo aula ...."** inamaanisha
A. ni jambo wazi
B. ni muhimu
C. si sawa
D. ni jambo la kweli

**47.** Mwandishi ametaja aina ngapi za elimu?
A. Mbili
B. Moja
C. Tatu
D. Tano

**48.** Ni nani hunufaika kutokana na elimu?
A. Aliye na elimu ya juu.
B. Anayepata kazi baada ya kuelimika.
C. Anayesoma kwa bidii.
D. Anayeandamanisha elimu na mienendo ifaayo.

**49.** Neno mwiko lina maana ipi?
A. Kifaa cha kusongea ugali
B. Jambo lisilokubaliwa
C. Tamaa
D. Jambo lisilofahamika

**50.** Toa mada mwafaka ya kifungu hiki
A. Elimu dunia
B. Ustaarabu
C. Elimu
D. Elimu mwafaka